Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Na Dhamana (CMSA)

# MCB BANK PLC

(Imesajiliwa nchini Tanzania chini ya Sheria ya Kampuni ya Tanzania namba 212 ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, Cheti Cha Usajili Namba 90216)

## TAARIFA KWA UMMA
## UTOAJI WA HISA STAHIKI 185,474,760 ZA BENKI YA BIASHARA MWALIMU KWA BEI YA SHILINGI 110 KWA KILA HISA, KATIKA UWIANO WA HISA MPYA TATU (3) KWA KILA HISA MOJA (1)

Benki ya Biashara Mwalimu inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 07 Novemba 2025, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, imeidhinisha Waraka wa Matarajio wa Benki ya Biashara Mwalimu kuuza hisa stahiki 185,474,760 kwa wanahisa wake kwa bei ya Shilingi 110 kwa kila Hisa, katika uwiano wa hisa mpya tatu (3) kwa kila hisa moja (1) aliyonayo mwanahisa.

**Taarifa ya utoaji wa Hisa Stahiki za Mwalimu Commercial Bank PLC:**

| **Mtoaji** | **Mwalimu Commercial Bank PLC** |
|---|---|
| **Bei** | Shilingi 110 kwa kila hisa |
| **Idadi ya hisa zinazotolewa** | Hisa 185,474,760 |
| **Mtaji unaokusudiwa kukusanywa** | Shilingi 20,402,223,600 |
| **Uwiano wa hisa stahiki** | Hisa mpya 3 kwa kila hisa 1 aliyonayo mwanahisa |

Wanahisa wanashauriwa kusoma Waraka wa Matarajio utakaotumwa kwao. Uwekezaji unafanyika kwa kujaza Fomu ya Maombi inayopatikana kupitia tovuti ya Mwalimu Commercial Bank PLC www.mwalimubank.co.tz ; kupitia ofisi za Chama Cha Walimu (TTU); kwa mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam waliopewa leseni na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); au kupitia tovuti ya Mshauri Kiongozi www.itrust.co.tz Barua Pepe: mcbrightsissue@itrust.co.tz Simu: +255 659 071 777.

Maombi yatakamilishwa kwa kufanya malipo katika akaunti za Mwalimu Commercial Bank PLC zilizoorodheshwa hapa chini:

**AKAUNTI ZA MALIPO:**

1. **Malipo kwa Njia ya Benki**

| **Jina la Benki** | **Mwalimu Commercial Bank PLC** |
|---|---|
| **Jina la Akaunti** | MCB RIGHTS ISSUE COLLECTIONS |
| **Namba ya Akaunti** | 0000013101 |

2. **Malipo kwa Njia ya Lipa Namba (Mixx by Yas)**

| | |
|---|---|
| Mtandao | Mixx by Yas (Tigo) |
| Jina la Lipa Namba | MCB RIGHTS ISSUE |
| Lipa Namba | 00144 |

3. **Malipo kwa Njia ya Mawakala wa Tigopesa (Mixx by Yas)**

Kwa wanahisa wanaotumia mitandao mingine, malipo yanaweza kufanyika kupitia kwa mawakala wote wa Tigopesa (Mixx by Yas) wanaopatikana nchi nzima.

**Angalizo: Wanahisa wanakumbushwa kuweka CDS Namba yao wakati wa kufanya malipo.**

**Tarehe za Matukio Muhimu:**

| **Na.** | **Tukio** | **Tarehe** |
|---|---|---|
| 1. | Tarehe ya mwisho kununua Hisa | Jumanne, 18 Novemba 2025 |
| 2. | Tarehe ya Rekodi | Ijumaa, 21 Novemba 2025 |
| 3. | Usambazaji wa Fomu za Maombi kwa wanahisa | Jumatatu, 24 Novemba 2025 |
| 4. | Kufungua Mauzo ya Hisa Stahiki | Jumatatu, 24 Novemba 2025 |
| 5. | Kufunga Mauzo ya Hisa Stahiki | Ijumaa, 19 Desemba 2025 |
| 6. | Tangazo la matokeo ya Mauzo ya Hisa | Jumatatu, 05 Januari 2026 |
| 7. | Wasilisho la Rejesta kwa CSDR | Jumatatu, 05 Januari 2026 |
| 8. | Kuorodheshwa kwa Hisa DSE | Jumatatu, 12 Januari 2026 |

Wanahisa wanashauriwa kuwasiliana na mawakala wa Soko la Hisa la Dar es Salaam wenye leseni kutoka Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); wahasibu, wanasheria au washauri wengine wa masuala ya fedha kwa ushauri elekezi ili kufanya maamuzi sahihi ya uwekezaji.

**Imetolewa na:**

**Afisa Mtendaji Mkuu,**
**Mwalimu Commercial Bank Public Limited Company,**
**Barabara ya Sam Nujoma,**
**S.L.P 61002,**
**Dar es Salaam, Tanzania.**

**TAREHE: 14 Novemba 2025**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa kanuni za Mamlaka za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.